JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI

MPANGO WA UENDESHAJI SERIKALI KWA UWAZI WA MANISPAA YA KIGOMA UJIJI

(OGP SUBNATIONAL PILOT PROGRAM)

RASIMU YA MPANGO KAZI WA KWANZA

2016/17 – 2017/18

OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA
S.L. P 44
KIGOMA – TANZANIA **JULAI, 2016**

MAANA YA VIFUPISHO

OGP	Open Government Partnership
MD	Municipal Dierector
MICTO	Municipal Information Communication Officer
MUPO	Municipal Urban Planning Officer
MEPO	Municipal Economy and Planning Officer
MT	Municipal Treasurer
MEO (P)	Municipal Education Officer (Primary)
MEO (S)	Municipla Education Officer (Secondary)
MMO	Municipal Medical Officer
MHS	Municipal Health Secretary
MWE	Municiapl Water Engineer
MIA	Municipal Internal Auditor
MPO	Municipal Procurement Officer
IRM	Independent Reporting Mechanism

MPANGO WA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KWA UWAZI WA MANISPAA YA KIGOMA UJIJI

RASIMU YA MPANGO KAZI WA KWANZA
2016/2017 – 2017/2018

1.0 UTANGULIZI

Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership - OGP) ni juhudi ya kimataifa inayolenga kuhimiza uwazi, kuwawezesha wananchi kupambana dhidi ya rushwa na kuhimiza kutumia teknolojia mpya na kuboresha utawala bora. OGP ilizinduliwa rasmi tarehe 20 Septemba 2011 Mjini New York na nchi 8 wanachama waanzilishi. Nchi hizo ni Brazili, Indonesia, Mexico, Norway, Philippino, Afrika Kusini, Uingereza na Marekani.

1.1 UENDESHAJI WA OGP

OGP inasimamiwa na Kamati ya Uendeshaji ya Kimataifa ya wadau mbalimbali yenye wawakilishi wa serikali na asasi za kiraia. Miongoni mwa manufaa ya OGP ni kuboresha utoaji wa huduma na kufanya serikali ziwe na majukumu na kuwajibika zaidi kwa raia wao.

1.2 TANZANIA KUJIUNGA NA OGP

Tanzania ilijiunga na mpango huu wa Kimataifa mwezi Septemba 2011. Toka ilipojiunga, Tanzania imendelea kushuhudia mabadiliko ya kuongezeka kwa Uwazi na Uwajibikaji katika sekta mbalimbali. Mabadiliko hayo yanaonekana katika utoaji wa huduma, ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi na mipango ya Serikali, mapambano dhidi ya rushwa na uendelezaji wa masuala ya teknolojia nchini.

1.3 UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA OGP TANZANIA

Utekelezaji wa OGP unaenda sambamba na uandaaji wa Mpango kazi na kuweka ahadi za utekelezaji (Action Plan and Commitments). Mpaka kufikia sasa, Tanzania tayari imeshaandaa Mipango kazi miwili. Mpango kazi wa awamu ya kwanza wa Tanzania (2012 – 2013), uliweka kipaumbele kwa sekta za Elimu, Maji na Afya. Mpango Kazi wa awamu ya pili (2014/15 – 2015/16) utaendeleza vipaumbele vya sekta za Elimu, Maji na Afya na pia zimeongezwa sekta za Habari, Ardhi, Bajeti, Takwimu na Viwanda. Sekta hizi zina umuhimu mkubwa kwa wananchi katika nyanja za kijamii, kiuchumi na kisiasa katika kujenga utawala bora nchini.

1.4 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA OGP TANZANIA

Utekelezaji wa mpango wa OGP bado haujawa na mafanikio makubwa sana kwa sababu haujaweza kutekelezwa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijijini ambako walengwa hasa ndiko waliko. Kwa umuhimu wake, OGP imeona kuna kila sababu ya kuupeleka mpango huu katika ngazi hizi. Ili kufanikisha lengo hili, OGP ikaja na mpango mpya kwa Miji iliyochini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa za nchi wanachama unaojulikana kama ***OGP Subnational Pilot Program.***

OGP Subnational Pilot Program ndilo chimbuko la Manispaa ya Kigoma Ujiji kujiunga na Mpango huu wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi.

2.0 KUJIUNGA KWA MANISPAA YA KIGOMA UJIJI KATIKA OGP

Mwezi Februari 2016, OGP ilitoa tangazo ikilenga Miji iliyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuomba kujiunga. Miji 45 duniani ilituma maombi ya kujiunga na baada ya mchujo, Miji 15 zilikidhi vigezo vya kujiunga ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki na kati, ni Miji 2 tu ndio iliyoomba na kukidhi vigezo ikiwemo Mji wa Elgeyo Marakwet (Kenya).

Miji mingine duniani iliyokidhi vigezo hivyo na kujiunga na ***OGP Subnational Pilot Program*** ni kama ifuatavyo;

Buenos Aires (Argentina), Sao Paulo (Brazil), Austin (Marekani), Madrid (Hispania), Seoul (Korea Kusini), Ontario (Canada), La Libertad (Peru), Jalisco (Mexico), Paris (Ufaransa), Scotland (Uingereza), Sekondi-Takoradi (Ghana), Tbilisi (Georgia) na Bojonegoro (Indonesia).

2.1 UTENDAJI KAZI WA OGP

OGP inafanya kazi kwa kuzingatia Mpango kazi na ahadi za utekelezaji wa taasisi husika. Mapango kazi unakuwa wa mwaka mmoja kwenye sekta zilizochaguliwa kutekelezwa. Mpango kazi unaokubalika ni lazima utengenezwe kwa kushirikisha taasisi binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Asasi za Kiraia, Wanahabari na Serikali (Halmashauri).

Pia, OGP imeweka utaratibu wa kujitathmini na mfumo huru wa utoaji wa taarifa (Self Assessment and Independent Reporting Mechanism – IRM). Mifumo hii imewekwa ili kupata taarifa sahihi juu ya utekelezaji wa Mpango Kazi na Ahadi.

3.0 RASIMU YA MPANGO KAZI WA KWANZA WA MANISPAA

Mpango wa kwanza wa Uendeshaji Shughuli za Serikali kwa Uwazi kwa Manispaa ya Kigoma Ujiji umezingatia vipaumbele vilivyowekwa katika Mpango kazi wa awamu ya kwanza na awamu ya pili wa Serikali ya Tanzania ambapo kwa ujumla wake vipo nane (8) ambavyo ni Elimu, Maji, Afya, Ardhi, Uhuru wa habari, Uwazi katika bajeti, Uwazi katika Takwimu na Viwanda. Kati ya vipaumbele nane, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji inapendekeza kuanza na Sekta Sita (6) za kiupaumbele kama ifuatavyo;

1. Sekta ya Elimu
2. Sekta ya Afya
3. Sekta ya Maji
4. Sekta ya Ardhi
5. Uwazi katika Bajeti na
6. Uwazi katika Takwimu

Kupitia Mpango huu wa Uendeshaji Shughuli za Serikali kwa Uwazi, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji imeandaa mpango kazi na kuweka ahadi ya utekelezaji kwa sekta za Elimu, Afya, Maji, Ardhi, uwazi katika bajeti na uwazi katika takwimu na utelezaji wa shughuli za sekta hizi zitawekwa wazi kwa matumizi ya Umma.

3.1.0 SEKTA YA ARDHI

Ardhi ni rasilimali muhimu sana kwa wakazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji na kwa watanzania kwa ujumla. Uwazi katika kushughulikia masuala yanayohusu ardhi ni moja ya ahadi muhimu inayowekwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji katika kuhakikisha haki inatendeka ili kuondoa migogoro inayosababishwa na kukoseka uwazi.

3.1.1 Ahadi ya Manispaa ya Kigoma Ujiji:

Kuandaa mpango wa kamambe wa Mji (General Planning Scheme), kuwa na maeneo yaliyowekwa alama za upimaji (Demarcated area) na taarifa zote zinazohusu ardhi kupatikana kwenye tovuti ya Manispaa ifikapo mwezi Julai 2017.

Ili kufanikisha haya, Manispaa itaweka wazi kila mwezi taarifa zifuatazo;

- Taarifa za ardhi yote iliyowekewa alama za upimaji, ardhi iliyopimwa, ardhi iliyopimwa na kutolewa hati
- Kuweka kwenye tovuti ya Manispaa Mpango kamambe wa Mji kwa ajili ya matumizi ya umma
- Taarifa za wamiliki wote wa ardhi kwenye Manispaa
- Taarifa za maeneo ya wazi kwenye Manispaa

3.2.0 SEKTA YA AFYA

Afya ni moja ya sekta zinazosimamiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji. Utoaji wa huduma bora za afya zinazozingatia misingi ya uwazi ni jambo linalotarajiwa na kila mkazi wa Manispaa hii. Ili kujenga uaminifu kwa wakazi wake, Manispaa imejipanga kuweka wazi kila taarifa inayohusiana na utoaji wa huduma ya afya.

3.2.1 Ahadi ya Manispaa ya Kigoma Ujiji

Taarifa za Mapokezi ya Madawa, Mgawanyo wa dawa kwa kila kituo cha afya, zahanati na Hospitali teule kuwekwa kwenye tovuti ya Manispaa kwa ajili ya matumizi ya umma ifikapo Julai 2017.

Ili kufanikisha haya, Manispaa itaweka wazi kila mwezi taarifa zifuatazo:

- Taarifa za mapokezi ya fedha kwa ajili ununuzi wa dawa na vifaa tiba na mgawanyo wake
- Taarifa za dawa na vifaa tiba zilizonunuliwa kwa Hospitali teule, Vituo vya Afya na Zahanati
- Taarifa za hali ya upatikanaji wa dawa katika Hospitali teule, vituo vya Afya na Zahanati
- Taarifa za idadi ya wagonjwa waliotibiwa katika Hospitali teule, Vituo vya Afya na Zahanati na aina ya magonjwa yaliyotibiwa zaidi.
- Taarifa za vizazi na vifo
- Taarifa za magonjwa ya mlipuko

3.3.0 SEKTA YA ELIMU

Elimu ni sekta yenye umuhimu wa kipekee. Ni sekta inayohudumia sehemu kubwa ya wakazi wa Manispaa ikihusisha Wazazi, Walimu, Wanafunzi na wadau wengine. Kwa ukubwa wake, utoaji

wa huduma kwa uwazi utasaidia kujenga imani kwa wadau hawa na hata kuwavutia wengine kuchangia ukuaji na utoaji wa elimu bora zaidi**.** Manispaa imejipanga kuweka wazi taarifa inayohusiana na utoaji wa huduma ya Elimu.

3.3.1 Ahadi ya Manispaa ya Kigoma Ujiji:

Taarifa za Sekta ya Elimu za Manispaa kuwekwa kwenye tovuti ya Manispaa kwa matumizi ya umma ifikapo Julai 2017.

Katika kufanikisha ahadi hii, Manispaa inakusudia kufanya yafuatayo:

- Taarifa za mapokezi ya fedha za elimu bure kwa kila mwezi na kila shule ya Msingi na Sekondari kuwekwa wazi
- Taarifa za matumizi ya fedha za elimu bure kwa kila mwezi na kila shule ya Msingi na Sekondari kuwekwa wazi
- Taarifa ya mapokezi ya fedha za miradi na matumizi mengineyo za sekta ya elimu kuwekwa wazi.
- Taarifa za idadi ya walimu, wanafunzi na watumishi wengine wasio walimu kwa kila shule kuwekwa wazi
- Taarifa ya idadi ya madarasa, ofisi, matundu ya vyoo, madawati, viti meza, nyumba za walimu na uwepo wa uzio, zikionesha mahitaji, zilizopo na upungufu kwa kila shule kuwekwa wazi
- Taarifa binafsi za kila shule ikionesha ukubwa wa eneo la shule na uwepo hati miliki ya ardhi
- Taarifa za matokeo ya mitihani mbalimbali na nafasi ya shule kitaifa, kimkoa na Manispaa

3.4.0 SEKTA YA MAJI

Maji ni uhai. Bila maji hakuna shughuli inayoweza kufanyika. Upatikanaji wa huduma ya maji unachochea ukuwaji wa shughuli za kiuchumi. Uwepo wa huduma ya maji unapunguza milipuko ya magonjwa ya kuambukiza kama kipindupindu na homa za matumbo. Huduma ya maji safi na salama inapaswa kuwafikia wakazi wote wa Manispaa ya Kigoma Ujiji kwa mgawanyo ulio wazi na unaofahamika kwa wakazi wote. Manispaa imejipanga kuhakikisha uwazi katika utoaji wa huduma ya maji unakuwepo.

3.4.1 Ahadi ya Manispaa ya Kigoma Ujiji:

Taarifa za utoaji wa huduma ya maji kwa Manispaa kuwekwa kwenye tovuti ya Manispaa kwa matumizi ya umma ifikapo Julai 2017.

Katika kufanikisha ahadi hii, Manispaa inakusudia kufanya yafuatayo:

- Kutoa taarifa za hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kila mwezi kwa kila mtaa
- Kuweka taarifa za mtandao wa maji kwa eneo lote la Manispaa
- Kutoa taarifa za mapato na matumizi ya fedha za miradi ya maji
- Kutoa taarifa ya vyanzo vya maji

3.5.0 UWAZI KATIKA BAJETI

Uwazi katika mchakato wa uandaaji wa bajeti ni nguzo muhimu katika uendeshaji wa taasisi kwa uwazi. Umuhimu uwazi katika bajeti unaanzia pale bajeti inapoanza kuandaliwa, inapopitishwa, wakati wa utekelezaji na mwisho wakati wa ukaguzi wa utekelezaji wa bajeti. Taarifa za mchako huu zinapokuwa wazi, wadau wengine watajitokeza na kutoa maoni na michango yao katika kuifanya bajeti husika kutekelezeka na hivyo kuboresha maisha ya walengwa.

3.5.1 Ahadi ya Manispaa ya Kigoma Ujiji:

Taarifa za bajeti ya Manispaa na taarifa za kila robo za kamati ya ukaguzi kuwekwa kwenye tovuti ya Manispaa kwa matumizi ya umma ifikapo Julai 2017.

Katika kufanikisha ahadi hii, Manispaa inakusudia kufanya yafuatayo:

- Taarifa ya bajeti ya mwaka kuwekwa wazi kwa matumizi umma
- Rasimu ya bajeti iliyoandaliwa na watalaam kuwekwa wazi kwa matumizi umma
- Rasimu ya bajeti iliyopitishwa na Baraza la Madiwani kuwekwa wazi kwa matumizi umma
- Bajeti ilipitishwa na Bunge kuwekwa wazi kwa matumizi umma
- Kuandaa Muhtasari wa bajeti iliyopitiwa na Bunge kwa ajili ya wananchi
- Mapitio ya nusu mwaka ya bajeti kuwekwa wazi kwa matumizi umma
- Taarifa za Mapato na Matumizi kuwekwa wazi kwa matumizi umma
- Taarifa za madeni kuwekwa wazi kwa matumizi umma
- Taarifa za ukaguzi kuwekwa wazi kwa matumizi umma

- Kweka kwenye tovuti ya Manispaa matokeo ya uwasilishaji wa taarifa za Halmashauri mbele ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa matumizi ya umma

3.6.0 UWAZI KATIKA TAKWIMU

Ujio wa teknolojia mpya umetoa nafasi nzuri na njia bora zaidi ya kukusanya takwimu, kuzichambua na kuwezesha takwimu kuwafikia watumiaji wengi kwa urahisi. Teknolojia mpya imewezesha watu wengi kuwa na uwezo wa kutumia intaneti kupitia simu zao za mikononi na vifaa vingine na hivyo kurahisisha upatikanaji wa habari na takwimu muhimu kwa umma. Kwa takwimu mbalimbali kuwa wazi kwa umma, wadau mbalimbali wameweza kutoa maoni na michango yao yenye lengo la kuboresha sera, kuongeza ushiriki katika ufuatiliaji na kutoa mrejesho kwa umma.

3.6.1 Ahadi ya Manispaa ya Kigoma Ujiji:

Kuanzisha mfumo wa uwazi wa takwimu zinazohusu Manispaa katika tovuti ya Manispaa ifikapo Julai 2017.

Katika kufanikisha ahadi hii, Manispaa inakusudia kufanya yafuatayo;

- Kuanzisha tovuti ya Manispaa ya Kigoma Ujiji
- Kuweka kwenye tovuti ya Manispaa takwimu za sekta ya Elimu, Afya, Maji, Ardhi zinazohusu matokeo ya mitihani, idadi ya walimu, wanafunzi, majengo, samani na matundu ya vyoo, mapokezi na ugawaji wa dawa, idadi ya kaya zeneye vyoo bora na zisizo na vyoo, utoaji wa hati za umiliki wa ardhi, ardhi yaliyopimwa, maeneo ya wazi. Kaya zenye huduma ya maji safi, idadi ya visima, matenki ya uvunaji wa maji ya mvua na sekta nyingine kama barabara, fedha, maendeleo ya Jamii, Utumishi na utawala na matukio yanyotokea kwenye mitaa ya Manispaa.
- Kuweka matangazo ya zabuni zote na taarifa za mikataba yote ilisainiwa ya Manispaa

4.0 HITIMISHO

Mpango kazi huu umeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau wote kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji (Serikali), Asasi za Kiraia, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wanahabari. Mpango kazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji utaanza kutekelezwa kuanzia mwezi

Julai, 2017. Taarifa za kila robo mwaka za utekelezaji mpango kazi huu zitawekwa kwenye tovuti ya Manispaa ya Kigoma Ujiji kwa ajili ya matumizi ya Umma.

Ni imani kubwa ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji kuwa, ahadi zilizowekwa kwenye mpango kazi huu, unatengeneza njia kuelekea kwenye Manispaa inayoendeshwa kwa uwazi na uwajibikaji katika utoaji huduma kwa umma.

RASIMU YA MPANGO KAZI WA KWANZA WA MANISPAA YA KIGOMA UJIJI

MPANGO WA UTEKELEZAJI NA UPIMAJI

Na	Sekta iliyochanguliwa	Ahadi	Shughuli	Mhusika	Viashilia	Muda wa utekelezaji	Upimaji		
							Kijani	Njano	Nyekundu
1	Sekta ya Ardhi	Kuandaa mpango kamambe wa Mji (General Planning Scheme)	Mpango kamambe kuweka kwenye tovuti	MUPO MICTO	Uwepo wa mpango kamambe wa Manispaa	Julai, 2017			
		Kutoa taarifa za alama za upimaji na maeneo ya wazi kwa Manispaa yote	Kuweka taarifa za maeneo yote yaliyowekewa alama za upimaji, yaliyopimwa na maeneo ya wazi	MUPO MICTO	Uwepo wa taarifa za maeneo yote yaliyowekewa alama za upimaji, yaliyopimwa na maeneo ya wazi	Julai, 2017			
		Kuandaa na kuweka tarifa za hati miliki za ardhi kwenye tovuti	Kuweka taarifa zote za hati miliki za ardhi	MUPO MICTO	Uwepo wa taarifa za hati miliki za ardhi	Julai, 2017			
2	Sekta ya Afya	Kutoa taarifa za mapokezi ya fedha na dawa na vifaa tiba, mgawanyo wa dawa, idadi ya vifo, vizazi, wagonjwa waliotibiwa na magonjwa ya mlipuko kila mwezi kwenye	Kuweka taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha, ununuzi wa dawa na vifaa tiba na mgawanyo wa dawa na vifaa	MMO MHS MICTO	Uwepo wa taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha, ununuzi wa dawa na vifaa tiba na mgawanyo wa dawa na vifaa	Julai, 2017			
			Kuweka taarifa za wagonjwa waliotibiwa, vifo, vizazi na milipuko ya	MMO MHS MICTO	Uwepo wa taarifa za wagonjwa waliotibiwa, vifo, vizazi na milipuko ya	Julai, 2017			

		tovuti ya Manispaa	magonjwa		magonjwa				
Na	**Sekta iliyochanguliwa**	**Ahadi**	**Shughuli**	**Mhusika**	**Viashilia**	**Muda wa utekelezaji**	**Upimaji**		
							Kijani	**Njano**	**Nyekundu**
3	Sekta ya Elimu	Kutoa taarifa zinazohusu masuala ya elimu kwa matumizi ya umma	Kuweka taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha za elimu bure na miradi mingine kwa kila shule	MT MEO (P) MEO (S) MICTO	Uwepo wa taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha	Julai, 2017			
			Kuweka taarifa za idadi ya wanafunzi, walimu na watumishi wengine kwa kila shule	MEO (P) MEO (S) MICTO	Uwepo wa taarifa za wanafunzi, walimu na watumishi wengine	Julai, 2017			
			Kuweka taarifa za idadi ya madarasa, ofisi, madawati, meza, viti, matundu ya vyoo na nyumba za walimu kwa kila shule	MEO (P) MEO (S) MICTO	Uwepo wa taarifa za idadi ya miundombinu kwa kila shule	Julai, 2017			
			Kuweka taarifa za matokeo ya mitahani na nafasi ya shule kitaifa, kimkoa na kiwilaya	MEO (P) MEO (S) MICTO	Uwepo wa taarif za mitihani	Julai, 2017			

Na	Sekta iliyochanguliwa	Ahadi	Shughuli	Mhusika	Viashilia	Muda wa utekelezaji	Upimaji		
							Kijani	Njano	Nyekundu
4	Sekta ya Maji	Kutoa taarifa zinazohusu huduma za maji kwa matumizi ya umma	Kuweka kwenye tovuti ya Manispaa taarifa ya upatikanaji wa maji, miradi ya maji, mtandao wa maji, mapato na matumizi ya fedha za miradi ya Maji.	MWE MICTO	Uwepo wa taarifa za sekta ya maji kwenye tovuti	Julai, 2017			
5	Uwazi katika Bajeti	Kutoa taarifa za bajeti na Kamati ya Ukaguzi kila robo mwaka	Kuweka kwenye tovuti ya Manispaa taarifa 5 za zinazohusu bajeti ya Manispaa (bajeti ya mwaka, bajeti iliyoandaliwa na watalaam, bajeti iliyopitishwa na Baraza la Madiwani, Bajeti iliyopitishwa na Bunge, Mapitio ya nusu mwaka ya bajeti)	MEPO MICTO	Uwepo wa taarifa 5 za bajeti kwenye tovuti ya Manispaa	Julai, 2017			

Na	Sekta iliyochanguliwa	Ahadi	Shughuli	Mhusika	Viashilia	Muda wa utekelezaji	Upimaji		
							Kijani	Njano	Nyekundi
			Kuweka kwenye tovuti ya Manispaa taarifa za Mapato, Matumizi na Madeni kila mwezi.	MT MICTO	Uwepo wa taarifa ya Mapato, matumizi na madeni kwenye Tovuti ya Manispaa	Julai, 2017			
			Kuweka kwenye tovuti ya Manispaa taarifa na Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAAC)	MIA MT MEPO	Uwepo wa taarifa na Maagizo ya Kamati ya Bunge	Julai, 2017			
6	Uwazi katika Takwimu	Kuanzisha mfumo wa uwazi wa takwimu zinazohusu Manispaa katika tovuti ya Manispaa	Kuanzisha tovuti ya Manispaa ya Kigoma Ujiji	MD MICTO	Uwepo wa Tovuti ya Manispaa	Julai, 2017			
			Kuweka takwimu za Elimu, Afya, Maji, Ardhi kwenye tovuti ya Manispaa	MICTO Mtakwimu	Uwepo wa takwimu za Elimu, Afya, Maji, Ardhi kwenye tovuti ya Manispaa	Julai, 2017			
			Kuweka Matangazo yote ya Zabuni na Mikataba	MPO MICTO	Matangazo ya Zabuni na Mikataba kuonekana kwenye tovuti	Julai, 2017			